

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI

Simu: +255-26- 2323201-7
Nukushi: +255-26-2323208
Barua pepe: nje@nje.go.tz
Tovuti: www.foreign.go.tz



Jengo la LAPF Ghorofa ya 6,
Barabara ya Makole,
S.L.P 2933,
40466 DODOMA.

Unapojibu tafadhali taja:

Kumb. Na: QB 3/754/01/6

19 Desemba 2018

Waheshimiwa Mabalozi na Wawakilishi wa Kudumu,
Balozi zote za Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

**YAH: UTARATIBU WA DIASPORA WA KITANZANIA KUJIUNGA NA MFUKO WA
HIFADHI YA JAMII TANZANIA (NSSF)**

Tafadhali husika na somo tajwa hapo juu.

Wizara imepokea barua kutoka Mfuko wa Hifadhi ya Jamii Tanzania (NSSF) kuhusu utaratibu unaotakiwa kufuatwa na Diaspora wetu juu ya kijiunga na huduma zinazotolewa na Ofisi hiyo. Tumefahamishwa kuwa Diaspora wanaweza kijiunga na Mfuko wa Hifadhi ya Jamii Tanzania kwenye Skim ya **NSSF HIARI AU WESTADI**.

Taratibu za kijiunga, namna ya kuchangia / kulipia pamoja na faida zinazopatikana kwa watumiaji wa huduma hizo, zimeelezwa kwa kina katika tovuti yao ya www.nssf.or.tz. Kwa wale watakaopenda kijiunga na huduma ya NSSF HIARI itawalazimu kufika katika tawi lolote la NSSF lililopo hapa nchini. Aidha, kwa wale watakaopenda kijiunga na Skim ya WESTADI wanaweza kujisajili kupitilia tovuti ya Shirika hilo.

Kwa Diaspora yoyote atakayehitaji kijiunga na huduma hizo awasiliane na Bw. Cosmas Sasi, mwenye simu namba +255767454017 barua pepe: csasi@nssf.or.tz au Bi.Halima Mgalla simu namba +255753059129 barua pepe: hmgalla@nssf.or.tz kwa ajili ya ufanuzi zaidi.

Kwa barua hii, mnaombwa kufikisha taarifa hizi kwa Diaspora walio katika maeneo yenu ya uwakilishi ili waweze kunufaika na huduma hizo.

Wizara inatanguliza shukrani za dhati kwa ushirikiano wenu.

Balozi Anisa K. Mbega
Kny : KATIBU MKUU

Nakala :

Mkurugenzi Mkuu

Mfuko wa Hifadhi ya Jamii (NSSF)

S. L. P 1322

DAR ES SALAAM